

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Simu: 202-884-1080
202-939-6125
Nukushi: 202-797-7408
Barua pepe: ubalozi@tanzaniaembassy-us.org

1232 22nd Street, N.W.,
WASHINGTON, D.C. 20037

Kumb.No. KBA 195/655/01/'A'

Juni 18, 2015


Bw. Ndaga Mwakabuta,
Rais,
Diaspora Council of Tanzania in America (DICOTA),
12300 Pierce st NE,
Blaine, MN 55434.

YAH: ARDHI YA UWEKEZAJI KWA AJILI YA WATANZANIA WAISHIO MAREKANI

Tunapenda kuwajulisha kuwa Ubalozi umepokea barua kutoka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu maombi ya ardhi ya Uwekezaji kwa ajili ya Watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora).

Hivyo basi, kwa barua hii tunaomba muwajulishe wanachama wa Jumuiya zenu wawasilishe maombi yao rasmi ya ardhi ya uwekezaji kupitia Ofisi za Ubalozi ili yaweze kuwasilishwa katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi. Zoezi hili litakuwa linaendelea mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya watanzania wote waishio nje.

Tunatanguliza shukrani zetu kwa ushirikiano wenu.


Swahiba H. Mndeme
Kny: **BALOZI**